FORM ONE HOLIDAYS KEYNOTE KISWAHILI 10 QUESTION PAPERS



FORM 1 HOLIDAYS KEYNOTE KISWAHILI TEN QUESTION PAPERS

Prefer Calling Amobi Group of Examiners

@ 0743 333 000 OR 0706 851 439

For Marking Schemes

N/B In Response to the Huge Costs Associated in Coming Up with Such/Similar Resources Regularly, We inform us All, MARKING SCHEMES ARE NOT FREE OF CHARGE. However Similar QUESTIONS, Inform of soft Copies, are Absolutely FREE to Anybody/Everybody. Hence NOT FOR SALE

by Amobi Group of Examiners.


CALL AMOBI GROUP OF EXAMINERS @ 0743 333 000 OR 0706 851 439 TO ACQUIRE :













FORM ONE HOLIDAYS KEYNOTE
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 01

UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma taarifa hii kisha ujibu Maswali

Wanafunzi walikuwa *wakiterema* kwa furaha katika ukumbi wa shule. Hii ilikuwa siku yao ya kwanza katika shule ya upili. Waliyasubiri kwa hamu kuu makaribisho rasmi ya mwalimu mkuu wa shule hii yenye sifa kem kem. Muda si muda mlango ulifunguliwa. Sauti zilizokuwa juu *zilinywea*. Wanafunzi wote waliyaelekeza macho mlangoni. Mwalimu mkuu aliingia. Alikohoa kidogo kulisafisha koo kisha akasema, " Wanafunzi wa kidato cha kwanza hamjambo?"

"Hatujambo mwalimu!" Tulijibu kwa pamoja.

"Ni furaha yangu kuu kuwakakaribisha katika shule hii ya kitaifa ya Fanaka.

Madhumuni ya kuwataka mtangamane hapa, fauka ya kuwakaribisha rasmi, ni kuwajulisha na kuwafahamisha mambo kadha. Maisha yenu ya badaye ni kama jengo, na jengo likikosa msingi imara na madhubuti hutetereka na hatimaye kuanguka.

Lengo la kimsingi la shule ni kuwakuza wanafunzi ambao, zaidi ya kufuzu vizuri katika masomo yao, watakuwa *vielelezo* kwa taifa zima. Ninajua mna furaha kubwa baada ya kuhitimu mtihani wa darasa la nane. Ni kweli kuwa kila mtu ana haki ya kuufurahia ufanisi wake, lakini tujue pia kuwa tamu ikizidi tamu huwa si tamu tena. Ninachomaanisha ni kuwa *inatujuzu* kukumbuka kuwa, baada ya sherehe kuna kazi pia. Ili muweze kuwa na furaha kama hii tena baada ya matokeo ya mtihani wa kidato cha nne, lazima muwe na bidii kuanzia mwanzo. Elimu ni kama safari na ni muhimu kuwa tayari mapema. Waswahili husema kuwa msafiri ni aliye pwani.

Ni matumaini yangu kuwa haitawachukua muda mrefu kutulia na kuyazoea maisha yenu mapya. Kutulia huko ni muhimu ili kuwawezesha kukabiliana na majukumu mazito na adhimu yatakayowakabili. Ili kuwasaidia katika kutulia na kujizoeza vyema kwenye mazingira haya mapya, kila mmoja atapewa mwelekezi wa kumwongoza na kumshauri kuhusu kanuni za shule pamoja na kumjuza sehemu mbalimbali ambako shughuli Fulani maalum huendeshwa. Baadhi ya sehemu muhimu mnazotakiwa kuzijua ni *maabara*. Mathalani, maabara ya Kemia, Elimu-Viumbe naFizikia. Aidha kuna chumba cha mafunzo ya tarakilishi. Kama mnavyojua, tunaishi katika karne ambapo maendeleo ya kisayansi ni nguzo kuu ya ufanisi wa maisha ya binadamu.

Ni muhimu kukumbuka siku zote kuwa shule yetu hii imejengwa kwenye misingi ya nidhamu kwa kutambua kuwa kijengacho mtu ni utu na tabia. Kila mwanafunzi anatarijiwa kuonyesha nidhamu ya hali ya juu kwa walimu, wafanyikazi wengine wa shule, *viranja* na kwa wanafunzi wenzako.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Ni lazima kila mwanafunzi ahakikishe kuwa amezingatia adabu na *mbeko* katika matumizi ya lugha, kuzifuata kanuni zote za shule na kujiweka katika hali nadhifu.

Yamkini wengi mmeyazoea maisha ya nyumbani, laini hivi sasa mtalazimika kukaa mbali na ndugu, rafiki na *aila* zenu. Hali hii mpya haipaswi kuwa sababu ya kuwatosa katika biwi la simanzi. Badala ya kuhuzunika, mnapaswa kufurahia kuipata fursa na *abra* hii ya kujipatia marafiki wapya wa rika lenu. Aidha, hii ni nafasi nzuri ya kukumbana na hali nyingine ya maisha ambayo itawawezesha kuupanua ufahamu pamoja na uzoefu wenu wa kimaisha. Marafiki utakaokutana nao hapa wanatoka sehemu mbalimbali za nchi yetu na kwa kushirikiana nao na kufanya usuhuba nao utajenga nguzo imara ya ushirikiano katika miaka ya usoni. Huu ni msingi muhimu wa ushirikiano katika kiwango cha taifa, na kiini cha utangamano mkubwa wa utaifa. Hata hivyo, sio marafiki wote ambao ni wazuri kwa sababu hakuna mchele ukosao ndume. Lazima muwe na uangalifu katika kuwachagua marafiki zenu. Ukishirikiana na rafiki mbaya lazima atakuathiri. Nadhani sote tunajua kuwa mcheza na tope humruka.

Ikiwa utakumbana na matatizo yoyote usisite kumwuliza mwelekezi wako. Aidha, ni muhimu kuwauliza wanafunzi wengine ambao wana tajiriba ya mambo haya hapa shuleni au hata walimu wenu. Usilifutike jambo linalokusumbua au *kukukalifu* moyoni kwa sababu mwishowe litakuletea madhara makubwa. Ni muhimu kukumbuka niliyotangulia kusema kuwa, nia yetu siyo kuwaandaa wanafunzi wanaomudu masomo pekee, bali kuwakuza watu waliokamilika kiakili na kiutu. Hali hii haiwezi kufikiwa ikiwa kila mmoja atajitenga kivyake. Sote tunaelewa umuhimu wa methali isemayo umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

Ningependa kumalizia kwa kutoa mfano mfano huu. Mimi binafsi huiona shule kama kuku anayeatamia mayai. Akiyaatamia vizuri na katika mazingira mema, yale mayai yatatoatoa vifaranga wengi na wenye mayumaini. Vifaranga hawa nao wataindeleza jamii ya kesho. Lazima sote tushirikiane kuhakikisha kuwa hakuna *mayai viza* katika shule hii yetu.

Katika kipindi kijacho cha siku tatu, mtapata fursa ya kujulishwa sehemu mbalimbali za shule yetu na kuwajua walimu wenu. Ni matumaini yangu kuwa baada ya kipindi hicho, kila mmoja wenu atakuwa tayari kuyaanza masomo yake kwa msukumo mpya na bidi kubwa. Kwa miaka mine ijayo tutakutana mara nyingi na kuzungumza mengi. Kwa mara nyingine nawapongeza kwa matokeo bora katika mtihani wenu wa darasa la nane. La kuwakumbusha tu ni kuwa ukilima pantosha, utavuna pankwisha.

Sasa mnaweza kurejea madarasani mwenu kuwasubiri walimu ambao watawapa maelekezo na maagizo zaidi. Asanteni.'

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

a) Toa kichwa mwafaka kwa kifungu hiki **(alama 1)**

b) Ni kwa nini wanafunzi walikuwa wakiterema? **(alama 1)**

c) Wanafunzi walijumuika katika ukumbi wa shule kwa sababu maalum. Zitaje **(alama 2)**

d) Taja mawaidha yoyote mawili ambayo mwalimu mkuu aliwapa wanafunzi. **(alama 2)**

e) Ni nini umuhimu wa nidhamu kwa maisha ya mtu? **(alama 2)**

f) Tambua methali zozote mbili zilizotumika katika kifungu hiki **(alama 2)**

g) Ni kwa njia gani shule huweza kulinganishwa na kuku aliyeotamia mayai? **(alama 2)**

h) Eleza maana; **(alama 3)**

i) Viranja

ii) Tarakilishi

iii) Maabara

SEHEMU B: MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Taja na ueleze aina mbili kuu za sauti za Kiswahili **(alama 2)**

b) Tambua na utoe mifano miwili ya aina mbili za ala za kutamkia **(alama 2)**

c) i) Eleza tofauti kati ya sauti ghuna na sauti sighuna. **(alama 2)**

ii) Onyesha sauti ghuna au sighuna kati ya hizi ulizopewa**.** **(alama 2)**

/k/:
/g/: .
/s/: .
/z/

d) i) Silabi ni nini? **(alama 1)**

ii) Taja aina mbili za silabi katika Kiswahili **(alama 2)**

iii). Onyesha miundo yoyote miwili ya silabi za Kiswahili. **(alama 2)**

e) Eleza maana; **(alama 2)**

(i) Kiimbo

(ii) Shadda

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

f) Tambua sifa tatu tatu za sauti zifuatazo: **(alama 3)**

i) /a/

ii) /p/

g) Andika neno lenye muundo ufuatao wa silabi KKKI **(alama 1)**

h) Taja na ueleze aina nane za maneno ya Kiswahili **(alama 4)**

i) Tambua aina za maneno katika sentensi ifuatayo: **(alama 3)**

Mwerevu sana anapumzika chini ya mti jijini

j) Bainisha kundi nomino na kundi tenzi katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Gari lile bovu liliondolewa barabarani

k) Tunga sentensi kwa kutumia nomino za ngeli zifuatazo: **(alama 3)**

KI-VI

LI-YA

U-ZI

l) Kanusha katika wingi: **(alama 2)**

Mwalimu alinunua karatasi na kalamu

m) i) Kirai ni nini? **(alama 1)**

ii)Bainisha virai katika sentensi ifuatayo **(alama 3)**

Darasa letu lina wanafunzi watiifu sana

n) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa **(alama 2)**

Mtoto ameabiri gari leo asubuhi

o) Andika methali inayoweza kutolewa kwa mtoto asiyesikiliza wazazi wake au wakubwa wake na baadaye akapata madhara. **(alama 1)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Sehemu ya C: Isimu Jamii **(alama 10)**

a) Lugha ni nini? **(alama 1)**

b) Kwa nini Kiswahili kinachukuliwa kuwa lugha? **(alama 4)**

c) Fafanua dhima/umuhimu wa Kiswahili katika jamii **(alama 5)**

Sehemu ya D: Fasihi Simulizi (alama 15)

a) Fafanua maana ya Fasihi simulizi **(alama 2)**

b) Fasihi simulizi ina umuhimu gani katika jamii? **(alama 5)**

c) Bainisha tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi **(alama 8)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS KEYNOTE
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 02

UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali yanayofuata

Madhara ya sigara

Chimbuko la kuonekana kwa madhara ya tumbaku ilikuwa mwaka 1598 A.D. Madhara yake yaligundulika wakati ambapo makala ya kwanza ya kiafya iliandikwa nchini Uingereza ikieleza madhara ya sigara. Baada ya hapo zilifuatia tafiti mbalimbali zilizoendelea kugundua na kuelezea madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa za tumbaku kwa binadamu. Matokeo ya tafiti hizo yaliwezesha baadhi ya nchi kama vile Denmark, Uholanzi na Sweden kutunga sheria zinazozuia matumizi ya sigara. Katika sura ya pili, baadhi ya serikali zilikwazwa kiuchumi kwa kukosa pato la kodi zitokanazo na sigara na bidhaa zingine za tumbaku.

Mashirika na kampuni zinazojishughulisha na uzalishaji na uuzaji wa sigara hutenga fungu kubwa la fedha kwa ajili ya kutangaza bidhaa hiyo hatari kwa afya ya mwanadamu. Kila mwaka, Shirika la Afya Ulimwenguni hutenga siku maalumu ya kuelimisha jamii kuhusu athari za kiafya na madhara yatokanayo na matumizi ya tumbaku. **Maadhimisho** hayo hufanyika kila Mei 30 ya mwaka na kauli mbiu ya mwaka huu ilikuwa "Mkinge mwanamke kuwa mteja au kutumiwa kama mhamasishaji wa bidhaa zingine za tumbaku'.

Takwimu za shirika hilo zinabainisha kuwa asilimia 90 ya wavutaji sigara wameanzia umri wa miaka 18. Pia zimebainisha kuwa, kwa kila sekunde ipitayo, wastani wa mtu mmoja anafariki kutokana na madhara ya tumbaku. Inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2025, vifo vitaongezeka kwa asilimia 70. Utafiti umebainisha ifikapo mwaka 2030, watu milioni 10 watakuwa wamefariki kutokana na kuvuta sigara.

Uvutaji sigara unasababisha magonjwa mengi kama vile saratani ya mapafu, wendawazimu, **kupooza,** matatizo ya mfumo wa hewa, kutoboka utumbo, kunyonyoka nywele, kupungua kwa nguvu za kiume, maradhi ya ngozi na kadhalika. Madhara ya tumbaku hayajitokezi mara moja. Huchukua kipindi kirefu hata miaka 30, hali inayowafanya wengi kufumbia macho tahadhari iliyopo, wakiendelea kuteketezwa na uvutaji sigara. Anayevuta sigara huathirika mapafu kutokana na moshi na tindikali – aina ya kaboni iliyomo kwenye tumbaku inayomzuia kupumua na mapafu yake huanza kutunga usaha. Hali hiyo huchangia mtu kupata athari nyinginezo kama

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

vile kichomi, kifua kikuu na saratani. Chembechembe ya nikotini iliyomo katika tumbaku ni hatari kwa mvutaji kwani humpotezea mtu hamu ya kula na anapata maumivu makali ya tumbo.

Wakati wote, mvutaji sigara hutoa harufu mbaya mdomoni, hali ambayo haipendezi katika maisha ya mwanadamu, na pia, huwa anawadhuru wengine. Mtu huyo anapopumua huchafua mazingira kwa kupumua hewa chafu na mbaya zaidi ambayo huwadhuru watu walio karibu naye kama vile mwenza katika ndoa (mke au mume), watoto au marafiki.

Inaelezwa kuwa sigara huathiri akili ya mwanadamu kutokana na kuwepo kwa chembechembe za ulevi. Hali hiyo ipo zaidi mtu anapotumia sigara kwa mara ya kwanza kabisa. Utafiti wa kitaalamu umethibitisha watoto wanaolelewa katika mazingira ya wazazi wanaotumia sigara kuathirika mishipa inayosafirisha damu kwenda katika moyo. Hali hiyo husababisha kuharibika kwa mfumo wa usafirishaji damu mwilini kwa watoto hao na mwishowe wanakuwa wahanga wa maradhi tofautitofauti.

Katika sura ya pili ya kisaikolojia, watoto wanaokaa na wazazi wanaovuta sigara huishia kuifuata tabia hiyo na huo ndio huwa mwanzo wa kudhoofika kwa maadili. Kwa wajawazito, sigara ina madhara kama vile kuathiri ukuaji wa mimba na kondo la nyuma au *placenta* kwa Kiingereza na kushindwa kusafirisha chakula vizuri kutoka kwa mama kwenda kwa moto. Madhara mengine ni moto kuzaliwa na uzito pungufu, hivyo kuathiri ukuaji wake. Kwa hivyo, ni vyema kufahamu kuwa ingawa sigara ni bidhaa inayotumiwa kama uraibu wakati wa kuivuta, madhara yake ni janga kubwa linalopaswa kupigwa vita bila kuchoka.

Maswali

(a) Madhara ya sigara yalionekana mwaka gani ? **(alama 1)**

(b) Ni nchi gani zilizokuwa za kwanza kubuni sheria mpya kuhusu uvutaji wa sigara ? **(alama 1)**

(c) Uvutaji wa sigara una athari gani kwa anayevuta ? **(alama 5)**

(d) Watoto wanaathiriwa vipi na sigara ? **(alama 4)**

(e) Thibitisha kwamba uvutaji sigara hugharimu pesa nyingi. **(alama 2)**

(i) Kupooza

(ii) Maadhimisho

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

LUGHA - SEHEMU B

(a) Kwa kuzingatia jinsi ya kutamka sauti za kswahili ni nini tofauti kati ya **(alama 2)**

(i) Irabu

(ii) Konsonanti

(b) Eleza maana ya dhana hizi **(alama 2)**

(i) Kiimbo

(ii) Shadda

(c) Taja vipashio vine vya lugha **(alama 4)**

(d) Andika sentensi zifuatazo katika hali timilifu **(alama 2)**

i) Mabati yananunuliwa

ii) Baba atakwenda dukani

(e) Kanusha sentensi zifuatazo **(alama 3)**

(i) Nchi za Afrika mashariki zalemewa na madeni.

(ii) Mbu amemuuma mtoto.

(iii) Baba ameandika barua ndefu.

(f) Zigeuze sentensi zifuatazo ziwe katika wakati uliopita (alama 2)

(i) Unapendelea kula nyama siku hizi.

(ii) Opiyo alipenda kujiingiza katikati kama mchuzi wa ugali.

(g) Andika kwa wingi **(alama 2)**

(i) Maziwa ya mtoto yalimwagwa na paka yule.

(ii) Uvivu wa Juma unakera.

(h) Akifisha sentensi zifuatazo (alama 2)

(i) nenda sokoni ukaninunulie sukari maziwa na mkate

(ii) Maadam umeshafika tuanze mkutano

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

(i) Kamilisha jedwali lifuatalo kwa kuandika viambishi mwafaka kulingana na kitenzi **(alama 5)**

Kitenzi	Nafsi	Wakati	Kirejeshi	Kitendwa	Mzizi	kiishio
Aliyelima						
Aliyempiga						
Anaoupanda						
Alipika						
Nitavileta						

(j) Taja vipera vya fasihi simulizi **(alama 2)**

(k) Onyesha vielezi katika sentensi zifuatazo **(alama 2)**

Mama amepika chai tamu sana

Nitakutembelea kesho jioni

(l) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendwa **(alama 4)**

Piga - Jenga – Fagia – Chora -

(m) Taja na ueleze dhima ya lugha **(alama 2)**

(n) Andika sentensi zifuatazo katika hali ya mazoea **(alama 2)**

(i) Mchoraji yule anachora picha nzuri

(ii) Mpishi atapika chakula kitamu

(o) Bainisha maneno katika sentensi zifuatazo. **(alama 4)**

Salaala ! Majangili wamewaua ndovu kumi leo asubuhi

Wale watafungwa

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FASIHI (ALAMA 15)

Taja majukumu matano ya fasihi ya kiswahili **(alama 5)**

Taja tofauti ya fasihi simulizi na fasihi andishi **(alama 10)**

ISIMU JAMII (ALAMA 10)

Nunua sabuni mpya ya GRESHA. *It is new !* Harufu yake ni *poa,* inadumu siku yote, inalainisha ngozi. Ng'arisha nguo zako na sabuni ya GRESHA. GRESHA sabuni *poa !* Bei yake ni nafuu; shilingi 20/= tu. Kila mtu ainunua.

Maswali

(a) Hii ni lugha gani ? **(alama 2)**

(b) Eleza sifa za lugha hii. **(alama 8)**

Insha (Aalama 20)

Andika insha itakayomalizikia kwa maneno haya ……. "Nilipopokea mezani chakula kitamu nilikumbuka maisha magumu niliyoyapitia, nikatambua kuwa si rahisi kupata chakula kama hicho bila juhudi maishani."

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS KEYNOTE
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 03

UFAHAMU: (ALAMA 15)
Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

Gogo

Umezuka moto kweli, misitu yateketea,
Wachanji wameduwili, hakuna pa kukimbia,
Zimewakwama akili, mashoka yanaungua,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

Kwa kweli kila mahali, halaiki yaumia,
Si Kenya si Shelisheli, mamia yaangamia,
Shikeni yangu kauli, msije kujijutia,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

Ijapokuwa kalili, muda wa kuhadithia,
Yapimeni kwa ratili, haya ninayowambia,
Sijegeuka shubili, tamu mnayodhania,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

Moto huno ni kukuli, hauchomi kuchagua,
Hauna jaji wakili, kwamba utajitetea,
Huchoma kiwiliwili, pingiti likasalia,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

We mchanji kaa tuli, boresha yako tabia,
Kugwenya lile na hili, magongo kujsombea,
Twaja tujipige wali, siku ya kukufukia,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Ili wepuke muhali, usije kujililia,
Gogo ulo na kibali, chanja ulilozowea,
Usiyachanje mawili, zani utajibwagia,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

Maswali:

1. Shari hili ni la aina gani? **(ala 2)**

2. Eleza vina vya shairi hili. **(ala 2)**

3. (a) Eleza maana ya mizani? **(ala 1**

(b) Shairi hili lina mizani ngapi katika ubeti wa tatu mshororo wa kwanza? **(ala 1)**

4. Taja kibwagizo cha shairi hili . **(ala 1)**

5. Taja nchi mbili zilizotajwa katika shairi. **(ala 1)**

6. Mshairi ametumia uhuru wa kishairi. Eleza huku ukitolea mifano kila maelezo. **(ala 4)**

7. Eleza maana ya msamiati ufuatao: **(ala 1)**

- Pingiti –
- Zani –

8. Eleza ujumbe unaowasilishwa na mshairi. **(ala 1)**

SARUFI: ALAMA 25

1. Pambanua sauti hizi kama ni ghuna au sighuna. **(ala 1)**

/s/ /z/

2. Eleza maana ya shadda. **(ala 1)**

3. Tia shadda kwenye maneno yafuatayo ili kuleta maana iliyo katika mabano.

Ala (kifaa)

Ala (mshangao)

Barabara (njia kuu)

Barabara (sawasawa) **(ala 2**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

4. Toa mifano miwili ya aina za kamusi. **(ala 1)**

5. Tunga sentensi moja ili kutofautisha maana ya maneno yafuatayo pafu and bafu. **(ala 1)**

6. Taja vipashio vya lugha. **(ala 2)**

7. Andika maneno yenye miundo ya silabi ifuatayo;

KKKI

II **(ala 1)**

8. Bainisha maneno katika sentensi zifuatazo.

Kitabu kimeanguka chini ya meza. **(ala 2)**

9. Taja na ueleze aina mbili za viambishi. **(ala 2)**

10. Jaza viambishi vinavyofaa katika nafasi.

i) Mitikiti _____liyopandwa juzi ____ mimea. **(ala 1)**

11. Ainisha viambishi katika sentensi ifuatayo: **(ala 3)**

Walitupongeza.

12. Taja sifa mbili za lugha. **(ala 2)**

13. Onyesha matumizi ya alama zifuatazo za uafikishaji. **(ala 2)**

Mshazari –

Koloni –

14. Yaweke maneno yafuatayo katika ngeli mwafaka: **(ala 2)**

a) Sukari –

b) Chuma –

15. Onyesha matumizi mawili ya kiimbo. **(ala 2)**

ISIMU JAMII: (ALAMA 10)

I. Eleza kaida za lugha. **(ala 4)**

II. Taja sifa za sajili ya shuleni. **(ala 6)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS KEYNOTE
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 04

SEHEMU YA A: INSHA (ALAMA 20

1. Tunga kisa kitakachomalizikia kwa maneno yafuatayo

…….hadi leo jitihada zangu za kuweka kumbukumbu za tukio hilo katika kaburi la sahau zimekuwa kama dau la mnyonge ambalo haliendi joshi. Hazifanikiwi.

SEHEMU YA B: UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali

Kamusi ya Kiswahili inafasili neno 'dawa' kama 'kitu kinachopewa mtu ili apone ugonjwa alio nao." Neno 'dawa' pia hutumiwa kumaanisha kitu kinachopumbaza au kutia sumu au kuzua tumbuizo kwa kuduwaza akili. Kwa mfano, wataalamu wamefikia uamuzi kuwa pombe, kwa mazoea, hutuliza ubongo wenye uchovu ilihali bangi hutuliza maumivu na kusababisha kusinzia; nayo majani ya mti unaotumiwa kutengeneza kokeini, hufisha ganzi na kumwezesha mtu kuvumilia uchungu au uchovu.

Na je, uraibu ni nini? Uraibu ni hali ya kuzizoeza au kutumia kitu mara kwa mara hadi kutegemea hicho ambacho mtu amekizoea. Kwa hivyo, uraibu ni mazoea ambayo mtumizi ameshindwa kuyaacha. Hali hiyo ya uraibu huanza kwa kitendo amabacho huonekana kana kwamba hakiwezi kamwe kumdhuru anayetumia dawa. Lakini, baada ya muda, fikira zake huanza kuzoea hivi kwamba, hata kabla ya mwili kuanza kutegemea dawa hiyo, akili huitarajia. Hii ni kwa sababu, punde baada ya matumizi, mtu huhisi hali ya utulivu ambao, kwa kweli, si wa hakika bali ni kama uliotiwa chumvi kwani hasa, hamna mashiko.

Kuna aina tofauti za dawa ambazo hutumiwa vibaya na watu. Baadhi ya dawa hizo huzua hisia za kumtia mtu chonjo isiyo ya kawaida. Zingine husababisha ulegevu ambapo mtumizi hihisi usingizi au 'ufu' bada ya uti wa mgongo kuathiriwa kasha mtu akakumbwa na hali ya usahaulifu halafu asiweze kufuatiliza fikira kwa mantiki kama kawaida ya binadamu mwenye akili razini hadi kufikia kupoteza fahamu.

Matokeo ya matumizi ya dawa zisizofaa huwa ni mtu kukumbwa na hali hiyo ambapo anajihisi 'akiwa juu" na hutamani mno kuendeleza hisia hizo hadi anapokuwa hajiwezi wala

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

kujimundu ndiposa watu huanza kumsema mtu kama huyo – kwamba amehusudu kupindukia hali hiyo ambapo, uraibu huwa umetimia.

Dawa za kulevya zinaweza kulinganishwa na kisu kinachotumiwa jikoni. Kisu hicho kina kazi maalum. Kazi yake ni kukata mboga kama kabeji, karoti, nyanya, vitunguu na vyakula kama mikate na vinginevyo. Lakini kisu chicho hicho kinaweza kutumiwa kumkata shingo binadamu! Basi hapo kitakuwa kimenajisiwa – yaani kutumiwa kwa njia isiyofaa.

Kila mara mtu anapomeza tembe au dawa yoyote yenye uwezo wa kusisimua sehemu ya mbele ya ubongo, mtu huyo huhisi msisimuko.

Bangi, miraa, pombe (kama chang'aa, busaa, muratina, kwete, kaluvu na zinginezo) na sigara zina mnato ambao humzuzua mtumizi hadi asiweze kujizuia na hata akapuuza mambo mengine muhimu angalau apate hisia hizo za kusisimua. Mtu kama huyu, ingawa anatambua kuwa anatumia dawa hizo, hatambui kamwe jinsi zinavyoathiri ubongo wake. Na jinsi zitakavyomdhuru siku za usoni.

Baadhi ya wanaouza dawa hizo kwa vijana huwa wanahoji: "Iwapo vijana hawa ni wajinga kufikia kiwango cha kujiruhusu kukubali kuharibiwa miili yao hivyo, basi name nitakuwa mjinga kama wao iwapo name sitatumia ujinga huo wao kujipatia faida."

Kwa nduli mwenye maoni kama hayo, wasia ambao tunaweza kumpa ni huu: iwapo haja yako kuu maishani ni kujipatia faida, basi tambua kwamba hucheka kovu asiyefikwa na jeraha. Na iwapo wewe ni mmoja wa wanaotumia dawa za kulevya na unaishi kwa mwelekeo wa kujistarehesha kwazo, basi umo kwenye hatari kubwa ya kuwa mtumwa wa hao wanaotafuta faida. Je, unafikiri umo duniani kwa haja ya kujitumbuiza huku ukidhuru mwenyewe?

Matumizi mabaya ya dawa za kulevya huathiri mwili, akili na roho. Kila mtu anapaswa kujali maslahi ya wenzake katika jumuiya anamoishi na kwa hivyo ni wajibu wa kila mtu kudumisha desturi yenye maadili na kuepuka kutumia dawa zinazovuruga akili na kudhoofisha mwili. Kwa kifupi, matumizi ya dawa za kulevya ni upumbavu mtupu.

Baadhi ya matokeo ya matumizi mabaya ya dawa ni hisia za pumbao la mawazo, kutojali mambo hatari, hamu ya kula kupindukia, ulegevu, vitendo vya kihuni, wasiwasi usio na sababu na hata wazimu. Matokeo mengine hasa ya dawa kama bangi, chang'aa, pombe na nyingine zinapotumiwa kwa wingi ni kwamba humfanya mtu asiweze kupumua vyema awe chonjo kuzidi kawaida, mkakamavu kuliko anavyopaswa, mwenye wasiwasi, anayesinzia kila mara, anayehisi kutapika, anayetetemeka viungo, anayeshuku watu kuwa wananuia kumdhuru, anayetenda

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

vitendo hatari kwake mwenyewe na kwa wenzake na hatimaye husababisha kupoteza fahamu na hata kufariki.

Mtu anapokolewa na dawa mwilini, tabia zake hudhihirisha kuchanganyikiwa akili, kutotambua baina ya hali halisi na hali inayotokana na fikira potofu, kutotambua wakati na kutojali lolote.

Maswali

(a) Teua anwani mwafaka kwa taarifa hii. **(alama 2)**

(b) Taja matokeo ya matumizi mabaya ya dawa za kulevya kwa mujibu wa kifungu hiki. **(alama 4)**

(c) Eleza vile walanguzi wa dawa za kulevya wanavyohalalisha vitendo vyao. **(alama 2)**

(d) taja dalili za kuthibitisha kuwa utumiaji wa dawa za kulevya amezidiwa na kiwango cha dawa mwilini. **(alama 3)**

(e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu. **(alama 4)**

(i) Duwaza

(ii) Fisha ganzi

(iii) Razini

(iv) Mnato

SEHEMU C: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

1. Andika sauti ambazo zina sifa zifuatazo. **(alama 3)**

(i) Irabu ya mbele juu

(ii) Kiyeyusho cha mdomo

(iii) Nazali ya ufizi

2. Huku ukitoa mfano eleza maana ya sauti mwambatano **(alama 2)**

3. Eleza miundo miwili ya ngeli ya U – ZI **(alama 2)**

4. Kanusha sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Nimemshukuru kwa kazi yake nzuri.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

5. Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mstari. **(alama 2)**

Sisi tutampata katika msitu.

6. Huku ukitoa mifano eleza matumizi ya viakifishi vifuatavyo. **(alama 2)**

(i) Kistari kifupi.

(ii) Kituo

7. Tumia 'O' rejeshi tamati katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Mwanafunzi ambaye hukosea mwalimu huadhibiwa.

8. Andika kwa ukubwa wingi. **(alama 2)**

Mji wetu umerembwa ukarembeka.

9. Tunga sentensi ukitumia kivumishi cha sifa pamoja na nomino katika ngeli ya A- WA. **(alama 2)**

10. Eleza maana ya: **(alama 2)**

(i) silabi

(ii) silabi funge

11. Yakinisha. **(alama 2)**

Mvua isiponyesha mimea haitanawiri.

12. Bainisha viambishi awali na tamati katika neno: (alama 2)

Tuliwapigia

13. Bainisha matumizi ya neno **vizuri** katika sentensi.

(i) Vitabu vizuri vimenunuliwa.

(ii) Anafanya kazi yake vizuri.

(iii) Vizuri vitanunuliwa na mwalimu.

14. Weka shadda kwenye neno lifuatalo ili kubainisha maana kwenye mabano. **(alama 2)**

(i) Ala (kifaa/zana)

(ii) Ala (kihusishi)

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

15. Sahihisha kwa njia tatu. **(alama 3)**

Mahali huku penu mna siafu.

16. Tunga sentensi moja ili kubainisha maana ya vitate. **(alama 2)**

(i) Kiza:

(ii) Kisa

17. Unganisha **(alama 2)**

(i) Kamau hali wali.

(ii) Kamau hali pure

18. Ainisha vihusishi katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Mimi niliwasili mapema kuliko wengine.

19. Chanda ni kwa kidole ilhali konde ni kwa **(alama 1)**

SEHEMU YA D: ISIMUJAMII (ALAMA 10)

1(a) Sajili au rejista ni nini katika isimujamii? **(alama 2)**

(b) Taja kaida zozote tatu za matumizi ya lugha. **(alama 3)**

2. X: Mmoja wenu afute ubao ili kipindi hiki king'oe nanga.

Y: Tafadhali…… naomba niulize swali kabla ya kuanzisha mada ya leo.

X: Uliza

(a) Tambua sajili ya makala uliyopewa. **(alama 1)**

(b) Taja sifa za sajili uliyotaja (alama 4)

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI (ALAMA 15)

1(a) Eleza maana ya ngano. **(alama 2)**

(b) Ngano zina umuhimu gani katika jamii? **(alama 5)**

2. Fafanua vipera vifuatavyo vya hadithi. **(alama 2)**

(i) Hekaya:

(ii) Hurafa:

3. Taja vipera viwili vya ushairi simulizi. **(alama 2)**

4(a) Eleza aina mbili za hadhira katika fasihi simulizi. **(alama 2)**

(b) Eleza sifa za mtambaji bora. (alama 2)

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS KEYNOTE
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 05

UFAHAMU ALAMA 15

Elimu

Ni dhahiri kabisa kuwa elimu ndiyo msingi wa maendeleo.Elimu ya ujuzi na maarifa humfaidi mtu kwa kila njia-kiuchumi, kisayansi, katika utafiti wa aina tofautitofauti na kwa kuinafidhi jamii kwa jumla.Bila elimu, maendeleo hayawezi kupatikana kamwe; kuyataraji ni kama kutumaini kupata kitu kwenye ombwe tupu.

Binadamu si kibonge au kidude kinachoweza kukaa bila chakula, mawasiliano na uhusiano kati yake na mazingira.Bila elimu, matatizo chungu nzima yatamkumba mwanadamu.Mifano ya matatizo haya ni kama vile ukosefu wa vyakula, hali duni ya mawasiliano, mmomonyoko wa udongo na hali nyingine za kuhuzunisha na kuaibisha.Maliasili yaweza kutumika tu iwapo pana ujuzi.

Mito, misitu na madini ni vitu ambavyo vinaweza kurahisisha mno maisha ya wananchi vikitumiwa kwa ujuzi.Kwa mujibu wa ukweli huu, kujua kusoma na kuandika, ambacho ndicho kiini cha elimu, ni jambo la lazima katika Maisha.

Elimu hurahisisha mawasiliano.Uwezo wa kupashana habari hutegemea ujuzi.Mawasiliano ni ya njia nyingi tofauti kama vile simu, barua, telegramu na njia nyingine.Nchi isiyo na mawasiliano bora ni kama jangwa lisilopitika.Kwa vile kila habari hugeuza hali Fulani ya Maisha, bila ujuzi wa kusoma na kuandika, mawasiliano hayawezekani.

Maandishi mengi huwa na uzito wa maana na mtu yeyote asiyejua kusoma na kuelewa hawezi kunufaika kupitia kwa maandishi ilhali ajuaye atasoma, aelewe na kutimiza wajibu wake wa ujenzi wa taifa.Wahenga walisema, fumbato mfumbie mjinga, mwerevu huling'amua, kwani mwenye macho haambiwi tazama.Ni wazi kwamba mwenye ujuzi wa kusoma na kuandika ndiye atakayeelewa mawazo ya wenzake yaliyoandikwa na kuyatumia katika harakati za ujenzi wa taifa.

Shuleni, wanafunzi hufunzwa kusoma na kuandika kusudi waweze kuchambua maandishi tofauti ili wawe na uwezo wa kujitegemea wenyewe kimaarifa.Kwa kuchambua maandishi tofauti, wanafunzi huelewa yale yafaayo na yasiyofaa katika jamii kwa kutumia mifano mizuri au mibaya ya wahusika katika kazi za kisanaa.Kwa njia hii, wanafunzi hupima kila hali kwa makini-yaani huwaza na kuwazua kabla ya kukata shauri kutenda lililo bora na la kuleta maendeleo.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Katika ulimwengu wa biashara, kujua kusoma na kuandika ni jambo muhimu kwa vile mfanyi biashara ni lazima achemshe bongo ili kazi yake isidhoofike na mwishowe aangamie kifedha.Ni lazima biashara itunzwe isije ikadidimia na ufukara ukaingia.Ufanisi katika biashara zifanywazo na watu binafsi huchangia ufanisi katika nchi kwa jumla, kwa maana haba na haba hujaza kibaba. Kupitia kwa utafiti katika nyanja tofauti, wanasayansi huwahudumia wananchi kwa njia nyingi madhubuti. Bila ujuzi wa kusoma na kuandika, watafiti, marubani, manahodha, madaktari na wahandisi na wenye taaluma nyingine hawawezi kupatikana.Kila mjuzi huwa na jukumu lake katika kuchangia maendeleo nchini; ni lazima mhandisi arekebishe mitambo, daktari atibu watu, nahodha aongoze chombo na mwalimu afundishe.Wote wanahitaji elimu.
Kwa mujibu wa hali hizi zote, ni Dhahiri kuwa ujuzi wa kusoma na kuandika ni jambo la lazima iwapo vikwazo katika ujenzi wa taifa vitaondolewa ili tupige hatua kubwa kimaendeleo.

Maswali

a) Je, elimu ina faida gani kwa mtu? **Alama 2**

b) Taja aina nne za shida zinazoweza kumkumba mtu kutokana na ukosefu wa elimu. **Alama 4**

c) Ni nini hasa kiini cha elimu? **Alama 2**

d) Eleza maana kamili ya mawasiliano na utaje mifano minne. **Alama 3**

e) Mwandishi anamaanisha nini anapotumia methali ‘fumbsto mfumbie mjinga, mwerevu huling’amua’? **alama 2**

f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika kifungu. **Alama 2**

Madini

Ombwe

MATUMIZI YA LUGHA ALAMA 35

a) Sauti hizi hutamkiwa wapi? **Alama 2**

/w/

/d/

b) Tofautisha kati ya irabu na konsonanti. **Alama 4**

c) Taja vikundi saba vya konsonanti kwa kutolea mfano ukizingatia hali ya mtetemeko katika nyuzi za sauti. **Alama 7**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

d) Kwa kupigia mstari, onyesha viambishi awali na tamati katika neno lifuatalo. **Alama 2**

Anakochezea

e) Taja vipashio vya lugha. **Alama 2**

f) Eleza maana ya**:** **Alama 4**

i) Shadda

ii) Kiimbo

g) Unda neno lenye muundo ufuatao. **Alama 2**

KKIKKI

h) Weka shadda mahali pafaapo. **Alama 1**

1) Marudio **2)** Karatasi

i) Eleza maaana ya maneno yafuatayo: **alama 3**

1) Kiambishi 2) Kihisishi 3) Kiwakilishi

j) Sahihisha. **Alama 2**

nelson mandela, aliyekuwa rais wa afrika kusini, alifanya mashauri na mobutu sesseseko wa zaire.

k) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika wakati ujao. **Alama 2**

Mpwa wangu anafua nguo zake.

l) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo. **Alama 2**

Mama anapika ilhali dada anaanika nguo.

m) Andika katika wingi **alama 2**

Baba anachimba kisima.

ISIMUJAMII ALAMA 10

Eleza majukumu yoyote matano ya lugha **alama 10**

FASIHI SIMULIZI ALAMA 20

1. Eleza dhima ya fasihi katika jamii. **(alama 10)**

2. Onyesha tofauti kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi **alama 10**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS KEYNOTE
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 06

UFAHAMU (ALAM 15)

Rita na Evelyn walikuwa marafiki wa chanda na pete kwa muda mrefu. Waliishi katika mtaa wa Kibokoni jijini Mombasa. Evelyn alikuwa mwanafunzi wa masomo ya uhazili katika chuo kimoja pale mjini. Naye Rita alifanya kazi ya ukarani papo hapo mjini. Waliishi kidugu katika chumba kimoja walichopanga pale mtaani.

Ingawa marafiki hawa walishirikiana kwa kila njia katika shughuli za upishi, kupiga deki, kufagia, kufua na kazi nyinginezo za nyumbani, aliyekuwa akitoa msaada mkubwa zaidi alikuwa ni Rita. Rita alikuwa na mazoea ya kutunza pesa zake vyema. Aidha alijua maana ya haba na haba hujaza kibaba. Alijua kuwa Evelyn, kama mwanafunzi, hakuwa na uwezo wa kuyakidhi baadhi ya mahitaji yake. Alijitolea sabili hata kumnunulia Evelyn nguo, viatu na vim vingine alivyohitaji. Mara nyingine ilibidi Rita kulipa kodi ya nyumba peke yake kwa vile mwenzake hangeweza kupata pesa kwa wakati. Hakuwahi hata siku moja kumkera wala kumtesa Evelyn kwa jinsi yoyote ile. Fauka ya hayo, hakuwahi kumsemesha vibaya wala kuonyesha dharau kwake. Aliamini kama wanavyosema watu kuwa dunia rangi rangile, huenda siku moja atahitaji kusaidiwa yeye pia. Siku kama hiyo atamtegemea Evelyn, mwandani wake.

Evelyn alipomaliza masomo yake alikuwa na bahati ya mtende. Alipata kazi nzuri mara moja katika kampuni moja ya maffita papo hapo jijini. Lakini muda si muda, mambo ya ajabu yalianza kutokea. Baada ya kupata kazi yenye kipato kizuri, kichwa cha Evelyn kilianza kufura mfano wa kaimati. Badala ya kunisaidia mwenzake katika kazi za pale nyumbani pamoja na gharama za maisha, alifhatilia raha za jijini kwa kuamini ule msemo wa ponda raha kufa kwaja. Rita alipomwuliza alimjibu kwa ukali, “Nikusaidie nini? Sasa si kama wakati nilipokuwa mwanafunzi. Kila mtu ana pesa zake.Ala!”

Rita hakumwelewa tena Evelyn.Isistoshe, alianza kumwibia Rita vitu vyake wakati alipokuwa hayupo nyubani. Mara kwa mara Rita aligundua kuwa pesa alizokuwa ameficha sehemu Fulani nyumbani zimedokolewa. Alipomwuliza, Evelyn alikujajuu, “Unafikiri mimi sina pesa? Unadhani ni wewe tu uliyeajiriwa?” Rita alizidi kushangaa, Muda wote alioishi na kumfadhili rafiki yake aliamini kuwa atamlipa mema. “Kumbe fadhila za punda ni mateke?” Alijiuliza Rita. Baada ya muda, urafiki wao ulivunjika na Evelyn akahamia mtaa wa Furaha alikoendelea na maisha yake ya starehe na ureda.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Hata hivyo mambo yalianza kumwendea mrama Evelyn. Wakubwa wake kazini hawakupendezwa najinsi alivyoendesha shughuli zake pale ofisini. Mara nyingi alifika kazini akiwa amechelewa na kila wakati alitoa vijisababu mbalimbali ambavyo havikumridhisha yeyote. Aidha, alipokuwa ofisini hakufanya mengi isipokuwa kutembea kutoka ofisi hii hadi nyingine akiwasumbua watu kazini mwao. Mara kwa mara alionekana akisinzia wakati wenzake walipokuwa wakichapa kazi. Lakini lililowakera zaidi wakuu wa kampuni hiyo ya mafuta ni jambo fulani lililoanza kutendeka pale. Vitu vya watu vilianza kupoteapotea.Mara mfanyikazi huyu anapoteza saa yake, mara mwingine anapoteza pesa, mara hiki mara kile. Wakuu walipoyatupa mawazo yao nyuma wakagundua kuwa mambo haya yalianza kutendeka mara tu alipowasili Evelyn. Wakaamua kumwekea mtego. Evelyn alioshikwa kimasomaso akidokoa mkoba wa msichana mwenzake. Mkoba huo ulikuwa umeaehwa juu ya dawati kimakusudi ili kumvuta Evelyn. Evelyn alifutwa kazi papo hapo. Fauka ya hayo, alitiwa mikononi na kukabidhiwa poisi waliomtupa korokoroni. Kesho yake Evelyn alifikishwa mahakamani na kushtakiwa kwa kosa la wizi. Alitozwa faini ya shilingi elfu tano au kifungo cha miezi sita. Hakuwa na pesa zozote za kulipia faini hii. Akawekwa rumande. Hata rafiki mmoja hakuwa naye wa kumuauni katika wakati huo wa majaribu.

Kwa bahati, Rita alisikia kuhusu kadhia hiyo.Hakupoteza muda. Akashika njia moja kwa moja hadi kituo cha polisi. Mpango ukafanywa na akamlipia. Evelyn ile faini. Evelyn alipoachiliwa hum akashangaa. “Yaani nimesamehewa ama nini?”Aliuliza.“La. Hujasamehewa.Faini uliyotozwa imelipwa na msichana yule.” Evelyn akageuka na kumwona Rita. Alimtazama kwa muda bila kujua la kusema. Mwishowe alimsogea kisha wakakaribiana polepole na kukumbatiana. Machozi yakaanza kumdondoka Evelyn, nde! Nde! Nde! Akalia kilio cha uchungu na soni. Akamwomba Rita msamaha, “Nisamehe, sikujua nililokuwa nikifanya.Nilidhani kuwa baada ya kupata kazi sitahitaji tena urafiki wako. Haya yaliyonipata yamenifunza,” alisema kwa masikitiko. “Evelyn, kijengacho mtu ni uth na tabia,” alisema Rita.“Ni kweli rafiki yangu” alitamka Evelyn, Sasa nimejitia kwenye shida.Hata kazi yangu nzuri nimeipoteza.Sina mahali pa kuishi. Itabidi nirudi kijijini kwa baba na mama. Kwaheri rafiki yangu naasante kwa yote uliyofanya.”“La! Hutaondoka”. Rita alimwambia lcwa dhati, “Tutakwenda nawe nyumbani mwangu tukaishi pamoja kama zamani. Nitayagharamia mahitaji yako yote hadi utakapopata kazi”.

Basi Rita na Evelyn wakaungana tena na kuishi vizuri katika nyumba ile ile mtaani Kibokoni. Kweli akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

MASWALI:

1. Maisha ya Evelyn na Rita yalikuwaje kabla ya Evelyn kupata kazi? **(alama 2)**

2. Kutokana na jinsi Rita alivyomtunza Evelyn, unafikiri yeye alikuwa ni mtu wa ama gani? **(alama 2)**

3. Eleza baadhi ya mambo ambayo Rita alimtendea mwenzake. **(alama 2)**

4. Baada ya kupata kazi Evelyn alikuwa mtu mkarimu. Je, unakubali?Eleza ilivyokuwa. (**alama 2)**

5. Evelyn alipokuwa mwanafunzi hakuwa na tabia ya udokozi. Unafikiri ni kwa nini alianza tabia hiyo baada ya kuajiriwa? **(alama 2)**

6. 'Asiyefunza na mama hufunzwa na ulimwengu.' Methali hii inahusianaje na Evelyn? **(alama 1)**

7. 'Akufaaye kiwa dhiki ndiye rafiki.' Methali hii inahusianaje na Rita? **(alama 1)**

8. Eleza maana ya misemo ifuatayo kama ilivyotumika kwenye kifungu: **(alama 3)**

(a) marafiki wa chanda na pete

(b) enda mrama

(c) jitolea sabili

SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 35)

1. Pambanua sauti hizi kama ni ghuna au sighuna. **(al 2)**

(i) /t/ (ii) /g/

2. Kamilisha methali zifuatazo; **(al 2)**

(i) Mgaagaa na upwa

(ii) Mvumilivu

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

3. Andika visawe vya ; **(al 2)**

(i) Janibu

(ii) Jadi

4. Tunga sentensi zenye maneno yafuatayo; **(al 3)**

(i) N + V + T

(ii) N + V + T + E

(iii) I + N + T

5. Onyesha viambishi awali na tamati katika sentensi hizi; **(al 2)**

(i) Alimkaribisha

(ii) Umeogelea

6. Onyesha matumizi manne ya koma**.** **(al 4)**

7. Maneno yafuatayo yako katika ngeli gani? (al 3)

(i) Mchungwa

(ii) Mdudu

(iii) Bonde

8. Andika sentensi zifuatazo katika umoja**.** **(al 3)**

(i) Nyavu zimechanikachanika

(ii) Nyuzi ziliingia matata

(iii) Fito zilikatwakatwa

9. Andika wingi wa**;** **(al 3)**

(i) Kiganja

(ii) Cheo

(iii) Kibindo

10. Geuza sentensi zifuatazo ziwe katika wakati ujao. **(al 2)**

(i) Mimi ninapenda mtoto mtiifu.

(ii) Ninyi mnapendwa na wenzenu.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

11. Geuza sentensi zifuatazo ziwe katika hali timilifu. **(al 2)**

(i) Safari hii itakuwa ndefu

(ii) Shamba letu linalimwa

12. Tunga sentensi ukitumia vitenzi hivi katika hali ya kutendewa. **(al 2)**

(i) Kata

(ii) Pasua

13. Eleza maana ya kirai. **(al 1)**

14. Onyesha kundi Nomino na kikundi tenzi katika sentensi hii**.** **(al 2)**

Hatibu hupaswa kuifahamu lugha

15. Tegua vitendawili vifuatavyo. **(al 2)**

Kisima kidogo kimejaa changararwe

Namsikia lakini simwoni

ISIMU JAMII (Al 10)

(i) Eleza maana ya sajili ya shuleni. **(al 2)**

(ii) Taja sifa nane za sajili ya shuleni. **(al 8)**

FASIHI SIMULIZI AL 10

1. **(a)** Fafanua maana ya ; **(al 2)**

(i) Fasihi andishi

(ii) Fasihi simulizi

(b) Onyesha tofauti zilizopo kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi. **(al 8)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS KEYNOTE
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 07

1. UFAHAMU

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali.

Asifuye mvua imemnyea. Hii ni semi yenye hakika isiyopingika, na kuitilia shaka ni sawa na kudai jua linaweza kubadilika na kuchomozea upande wa magharibi badala ya mashariki. Huu ndio ukweli uliodhihirika juzi katika vyombo vyetu vya magazeti.

Lisemwalo lipo na kama halipo linakuja. Waama, pafukapo moshi pana moto. Mwanafunzi mmoja wa kike kwa jina P.N. katika chuo kikuu kimojawapo nchini aliushangaza umma wa Kenya na ulimwengu kwa jumla alipodai kuwaambukiza wanafunzi wenzake wa kiume mia moja na ishirini na wanne virusi vya ukimwi.

Kisa na maana? Aliambukizwa ukimwi na mwanafunzi mwenzake aliyekuwa akifanya majaribio ya ualimu katika shule yao ya upili. Baada ya kushawishika sana alijuana naye kimwili, na matokeo yakawa kifo ambacho sasa alikuwa anawagawia wenzake.

Kisa kama hiki kinachangia kueleza kina kirefu cha kutamauka na upweke ambao maisha ya waja wengi yameingia kiasi cha kuwaacha wanyama ijapo wanaenda kwa miguu miwili bado. Katika mafunzo mojawapo ya kidini ambayo padre alinifunza mimi na wanafunzi wenzangu, tuliambiwa kisasi ni chake Mola, sisi waja yetu ni kushukuru tu. Mbona basi mwanafunzi kama huyu kutaka kulipiza?

Ima fa ima, na Waswahili husema, Mlaumu nunda na kuku pia." Huyu mwanafunzi hawezi kuachiwa atende alivyotenda. Aliyekula naye raha alikuwa mtu aliyefahamika vizuri sana kwake. Isitoshe, huenda wakati huo alikosana na mama na baba kwa kulala nje. Huenda alaikosana na ndugu zake kwa kukwepa nyumbani usiku wa manane kwenda kumwona huyu kalameni. Huenda alikosana na mwalimu wake kwa sababu kiburi kilianza kuingia. Kwa vyovyote vile, alikula raha na hastahili kuwaadhibu watu wasio na hatia kufidia makosa yake. Je, kama yeye na huyo jamaa wasingekuwa na ukimwi , raha kiasi gani wangezila hadi leo?

Jamii na watu wote kwa ujumla hawana budi basi kulaani vitendo vya P.N. vya kuwaambukiza wanafunzi wenzake virusi huku akijua. Hili ni kosa ambalo linastahili adhabu ya kifo. Dawa ya moto ni moto, na hatua inastahili kuchukuliwa haraka ili P.N. ambaye tayari amekiri hatia, atiwe nguvuni na adhabu itolewe.

Barua ya P.N. imefafanua jambo jingine sugu. Kwamba kiwango cha maadili katika vyuo vyetu kimezorota kiasi cha kufanyiana unyama usiosemeka. Vijana wengi siku hizi wanashiriki tendo la

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

ndoa nje ya ndoa bila haya. Huu upotovu wa maadili katika jamii wapaswa kushutumiwa na wote. P.N. hana sababu yoyote ya kibinadamu, kidini au kitu chochote kile kudai haki kwa uovu wake.

MASWALI

a) Ipe habari hii kichwa mwafaka. **(Alama 1)**

b) Katika aya mbili za mwanzo, mwandishi wa makala haya anamlaumu mwanafunzi kwa kosa gani? **(Alama 2)**

c) Eleza chanzo cha tabia za P.N. **(Alama 2)**

d) Mwandishi wa makala haya anapendekeza hatua gani ichukuliwe dhidi ya P.N. na kwa nini? **(Alama 3)**

e) Barua ya P.N. imeonyesha uvumbuzi mpya. Utaje. **(Alama 2)**

f) Taja tamathali moja ya lugha iliyotumika katika ufahamu na utoe mfano **(alama 2)**

g) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kama vilivyotumika katika taarifa. **(Alama 3)**

i) Ima fa ima

ii) Kufidia makosa yake

iii) kufanyiana unyama

MATUMIZI YA LUGHA

a) Kwa kuzingatia hali ya mtetemeko wa nyuzi za sauti, taja aina mbili kuu za sauti. **(alama 2)**

b) Fafanua muundo wa silabi katika neno Ngwena. **(alama 2)**

c) Tia shadda katika neno lifuatalo ili kutoa maana mbili tofauti. **(alama 2)**

Barabara

d) Taja vipashio nne vikuu vya lugha. **(alama 2)**

e) Tambua aina zozote tatu za sentensi kwa kuzingatia kigezo cha kiimbo **(alama 3)**

f) Karabati sentensi hii. **(alama 2)**

Mgeni ambaye aliyekuja atarudi kesho.

g) Kamilisha sentensi zifuatazo ukitumia neno lifaalo kutoka mabanoni **(alama 2)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

(i) Pahali ..... pana mali ..... (haba, hapa)

(ii) Harun aliiba pesa ..... akafikishwa ..... (kortini, kotini)

h) Bainisha matumizi ya mshazari katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Watoto/wazee walipewa zawadi/tuzo na askofu

i) Taja na utoe mifano ya aina mbili za nomino **(alama 2)**

j) Akifisha; **(alama 3)**

Mimi nimefurahi sana kuona kwamba umefika mapema je nikuandalie kinywaji gani.

k) Andika kwa wingi; **(alama 2)**

Kondoo huyu na mbuzi yule ni wa mfugaji yupi?

l) Kanusha sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Mimi nilienda dukani

m) Ni ala zipi za sauti zinazotumika kutamkia sauti zifuatazo? **(alama 2)**

(i) /b/ **(ii)** /th/ **(iii)** /v/ **(iv)** /g/

n) Bainisha maneno yaliyopigwa vistari **(alama 2)**

Kiatu chake kimeraruka

Cha kakao kimetafunwa na nguruwe.

o) Tunga sentensi kulingana na ngeli zilizotajwa. **(alama 2)**

U – YA.

I – ZI

p) Geuza sentensi katika kauli ya kutendwa.

Mama anapika chakula kitamu **(alama 2)**

q) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu **(alama 2)**

Dada ameenda sokoni

r) Tunga sentensi na uonyeshe kundi nomino na kundi tenzi **(alama 2)**

s) Tunga sentensi yenye upatanisho wa kisarufi ukitumia neno **kiroboto** **(alama 2)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

ISIMUJAMII (ALAMA 10)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

"Ndugu na madada, sote tumealikwa katika karamu hii ya Bwana. Kabla ya kujongea mezani pake, Bwana, pana haja ya kutakasa nyoyo zetu na kujutia madhambi yetu. Sisi sote ni watenda dhambi na inastahili kumwendea ili aweze kutuondolea madhambi yetu."

Maswali

a. Tambua muktadha wa dondoo hili **(alama 2)**

b. Eleza sifa zozote nne zinazojitokeza katika sajili hii **(alama 4)**

c. Umepewa nafasi ya kuzungumza katika mazingira haya. Taja sifa zozote nne za lugha ambazo ungetumia mbali na sifa zilizomo katika dondoo hili. **(alama 4)**

FASIHI SIMULIZI (ALAMA 15)

Soma Kifungu kifuatacho kisha ujibu Maswali.

Ghafla kama ajali, sungura alitokea katika kichaka kilichokuwa karibu, Macho ya mbwa ndiyo yalikuwa ya kwanza kumtua sungura huyo. Moyo wake ukamzaini kukitwaa kisungura hicho na kukonga roho yake. Mara alikumbuka onyo ambalo walikuwa wamepewa na malaika mkuu. Mvutano mkali ulizuka katika nafsi yake, 'Bwana wewe una njaa, vipi utakiacha kitoweo ambacho kwa kweli kinakunyoshea mkono?

i) Hiki ni kipera kipi? Kwan nini? **(alama 2)**

ii) Tambua sifa zozote nne za kipera hiki **(alama 4)**

iii) Eleza umuhimu wa kipera hiki. **(alama 5)**

iv) Fomyula ya kumalizia hadithi ina umuhimu gani? **(alama 4)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS KEYNOTE
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 08

SEHEMU I - INSHA **Alama 20**

Andika kisa kitakachoanza kwa maneno yafuatayo: kelele zilitanda usiku katika kijiji kizima …… Endeleza.

SEHEMU II UFAHAMU **(Alama 15)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali uliyoulizwa.

Ni dhahiri kwamba uharamia umechipuka kama desturi na mfumo wa maisha katika siku za hivi karibuni. Janga hili limeshamiri hususan pembeni mwa bara la Afrika Mashariki. Taarifa za uharamia zimetawala vyombo vya habari, kiasi cha kwamba haipiti siku bila kuripotiwa visa vipya vya matendo haya mabovu ambayo yanaweza tu kumithilishwa na uhayawani. Matukio haya yamewalimbikizia maharamia na nchi husika, simanzi na masaibu yasiyoweza kutiwa kwenye mizani.

Yumkini tatizo hilo halitokei pasi na kumotishwa na kitita kikubwa cha fidia kinachodaiwa na maharamia hawa. Aghalabu, suala hili lahusishwa pakubwa na azma na ari ya kuendeleza ujambazi wa kimataifa sawia na ulipuaji wa bomu mijini Nairobi na Dareslaam mnamo Agosti 7, 1998, na tukio la Septemba 11, mwaka wa 2001 kule Marekani. Maafa na uharibifu wa mali si hoja, la mno kwa maharamia ni kutosheleza matakwa yao. Kwa upande mwingine, ukosefu wa tawala- wajibika katika maeneno kunakotokea unyama huu ni thibitisho tosha la mazingira yanayowezesha na kuruhusu kuchipuka kwa janga hili.

Mchipuko wa baa la uharamia umelengwa jamii ya kimataifa ambayo ni mhudumu mkuu wa harakati kusitisha majanga makubwa kama vile njaa, umaskini na magonjwa yaliyosheheni pakubwa barani. Bila shaka, hili ni suala linaloshawishishwa na 'kinyume mbele.' Maharamia wanatishia utangamano wa kimataifa wanapotibua usafiri wa abiria na shehena zinazoelekezwa sehemu tofauti ulimwenguni.

Matumizi ya kidiplomasia na mashauriano hayaelekei kuzalisha matunda katika juhudi za kudhibiti uharamia. Zaidi ya hayo, matumizi ya nguvu yahusishayo mashambulizi pamoja na maharamia kufunguliwa mashtaka nchini Kenya na Ufaransa kunaelekea kupiga jeki juhudi za kukomesha uharamia ulimwenguni. Aidha, utawala wa nchi kunakochipuka uharamia haujajizatiti kuharamisha doa hili linalotisha ustawi wa kimataifa.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Mathalan, ni jambo lisilopingika inapobainika kuwa uharamia umedumaza biashara ya kimataifa hali inayochangia upungufu na ucheleweshaji wa bidha muhimu zinazoendeleza ustawi wa uchumi. Dosari hii inaelekea kukwamiza majowapo ya maendeleo ya milenia yanasisitiza uimarishaji na ushirikiano wa maendeleo ya upanuzi wa masoko ulimwenguni. Harakati za kitalii katika kanda ya Mashariki ya bara la Afrika zimehujumiwa. Na itakumbukwa bayana watalii hawasafiri tu kwa ndege bali hata kwa meli.

Jitihada za kuweka laini za mawasiliano chini ya bahari ili kurahisisha na kupunguza gharama za mtandao ulimwenguni ni ndoto ambayo haijatimia hadi hivi sasa, kufuatia juhudi za maharamia katika bahari ya Hindi. Kwa mujibu wa hali hii, mawasiliano mepesi na nafuu yasitarajiwe hivi karibuni. Licha ya hayo, shughuli za uvuvi na biashara nyinginezo kwenye kanda ya mwambao zimetiliwa shaka si haba. Itabidi mikakati na suluhisho la kudumu liweze kupatikana ili vitendo vya uharamia viweze kusitishwa.

a) Kwa nini uharamia umetamalaki ulimwenguni? **(alama. 3)**

b) Eleza madhara ya uharamia kwa jamii ya kimataifa. **(Alama 2)**

c) Uharamia unaelekea kumtia hofu mwandishi. Fafanua. **(Alama. 3)**

d) Fafanua juhudi zozote mbili zinazofanywa na nchi za kimataifa kukomesha uharamia. **(Alama 4.)**

e) Eleza maana yafuatayo kwa mujibu wa kifungu.

i Umechipuka

ii Dosari

iii Harakati

III SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

a) Taja irabu ya kati. **(Alama.1)**

b) Toa mifano miwili miwili konsontanti zifuatazo: **(Alama 4)**

i) Vikwamizo **ii)** Nazali

c) Kiimbo nini? **(Alama 1)**

d) Weka shadda panapofaa. **(Alama.2)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

i) Mkuu

ii) Kupatana

e) Taja vipashio vitatu vya lugha. **(Alama 3)**

f) Tambulisha aina mbalimbali za maneno katika sentensi ifuatayo. **(Alama 5)**

Mtoto Yule ameingia ndani ya shimo.

g) Badilisha sentensi zifuatazo ziwe katika hali ya wingi. **(Alama 4)**

i) Paipai hili lilinululiwa jana.

ii) Unyasi mrefu utakatwa kwa upanga.

h) Silabi ni nini? **(Alama 2)**

i) Andika neno lenye muundo wa : **(Alama 2)**

i) I + I

ii) K+ I+K+K+I

h) Onyesha viwakilishi (w) katika sentensi ifuatayo. **(Alama 2)**

Wote wawili walimwona huyo.

i) Kanusha sentensi zifuatazo. **(Alama 4)**

a) Yeye anaimba vizuri.

b) Nyumba kubwa itajengwa

j) Tunga sentensi moja moja kutofautisha maneno yafuatayo. **(Alama 2)**

a) Vua b) Fua

k) Eleza maana ya semi zifuatazo: **(Alama 2)**

i) Enda mrama

ii) Pata afueni

l) Onyesha kielezi (E) katika sentensi ifuatayo: **(Alama 1)**

Nyanya alitembea polepole.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

m) Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi ya alama ya nukta pacha.

n) Yakinisha sentensi ifuatayo. **(Alama 2)**

Maandishi yake hayaja pendeza mwalimu

o) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli uliyopewa mambanoni **(1)**

i) Futa(tendeka) ½

ii) Chagua (tendea) ½

SEHEMU YA IV: FASIHI SIMULIZI

a) Eleza majukumu matatu ya fasihi simulizi. **(Alama 3)**

b) Taja vipera vinne vya fasihi simulizi. **(Alama 4)**

c)i) Hekaya ni nini? **(Alama 1)**

ii) Eleza umuhimu wa hekaya. **(Alama 3)**

d) a) Hurafa ni nini? **(Alama 1)**

b) Eleza sifa tatu za hurufa. (Alama 3)

V) ISIMU - JAMII

a) Ni nini maana ya Isimu jamii? **(alama 2)**

b) Taja kaida nne za lugha **(alama 4)**

c) Eleza sifa nne za sajili ya hospitalini. **(alama 4)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS KEYNOTE
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 09

KISWAHILI KIDATO CHA KWANZA
MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA TATU,
MUDA: SAA 2.
SEHEMU A FAHAMU (ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali yafuatayo
sigara ni mojawapo ya uraibu ambao watu wengi san hushiriki. Kila uchao vijana wa kike na kiume hujitosa katika uraibu huu hatari kwa kujua au kwa kutojua. wengine huvutiwa kuvuta sigara kwa kulazimishwa na wenzao ili waweze kukubalika katika tabaka au kundi Fulani. ushawishi wa aina ndio hujulikan kama shinikizo – rika. Wengi hawafahamu madhara ya sigara kwa vile hayonekani moja kwa moja. Madhara yake huchukua muda mrefu kabla ya kuonekana au kudhihirika. Yanapofika kiwango hiki, mvutaji huwa amefikia uharibifu wa viungo vya ndani kwa hali ya juu. Si kupiga chuku ikisemekana kuwa mguu mmja huwa duniani na mwingine ahera

Madhara ya uvutaji sigara husbabishwa na kemikali zilizomo katika sigara. Sigara husheheni kemikali zaidi ya elfu nne. Nyingi za kaemikali hizi ni hatari na hudhuru. Kati ya zile zenye madhara makubwa kwa mwili wa mwanadamu an ambazo husababisha maradhi baada y kuvutwa kwa muda ni nikotini, hewa ya kaboni- monkasaidi na lami.

Kemikali hizi huingia mwilini kupitia kwa mapafu na kusababisha madhara mwilini. Baadhi ya maradhi ambayo husababishwa na uvutaji sigara ni pamoja na maradhi ya kansa, vidonda nya tumbo na shinikizo la damu. Shinikizo hili linaweza kuleta maradhi ya moyo na kupooza kaw mwili

Moshi wa sigara nao unapovutwa mwilini hingia na kugandama katika kingo za mapafu kama lami. Lami nayo huwa na sume kali anayoweza kuharibu mapafu. Umio na hufanya kuwa mwembamba ns sumu hii. Hii husbabisha kuweko kwa unyevu kama makamasi mengi. Ni muhimu kujua kuwa hata kupumua mishi wa sigara tu, kunaweza kudhuru afya yako.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Kwa kina mama wajawazito madhara ya moshi wa sigara huwa makubwa. Sigara inaweza kuharibu mimba au kufanya motto akazaliwa kabla ya wakati kutimia. Aidha, anaweza kuzaliwa akiwa wa chini sana. Hali hizi ni hatari kwa afya na maisha ya motto kama huyo.

Watemgenezaji wa sigara wanajua pasi na shaka madhara ya sigara kwa afya ya mwanadamu. Kwa kuzinagatia hili, onyo hutolewa kwenye pakiti za sigara kuwa uvutaji una madhara kwa afya yako. Hata hivyo, si wengi ambao hutilia maanani maonyo na tahadhari hizi. Lakini kwa huwa haja yao kubwa in pato, bado humarisha utengenezaji wazo. Si ajabu kusikia kuwa ni hatia kuuza sigara katika baadhi ya nchi, hasa zilizoendelea.

Makapuni ya kutengeneza sigara hutumia hila ili kuwavutia wavutaji wengi. Kwanza, matangazo hutolewa kwa njia nyingi za mawasiliano kama vile runinga, redio na magazeti.
Nayo hunadi Starehe kuu kwa wavuaji. Kwa kuwa wanajua madhara ya sigara, huweka onyo pembeni mwa pakiti kwa maadishi madogo sana yasiyoonekana vyema wala yasiyoivutia makini ya watu.

kunaya ni kuwa makampuni yanayotengeneza sigara ndiyo huongoza katika kuelimisha vijana walio chini ya miaka kumi na minane huhusu madhara ya sigara! Kinaya au uzandiki? huenda hii ni mbinu ya kuwahamasisha vijana kuhusu kuwepo kwa bidhaa zao ili wawe wateja wa siku za usoni. Uvutaji wa sigara unaweza kudhuru sio tu watu chini ya umri wa miaka kumi na nanem Mtu anapovuka miaka kumi na nane, bado ataathiriwa na uvutaji wa sigara! Ukweli ni kuwa uvutaji wa sigara una madhara mengi na husababisha magonjwa yanoyoangamiza tuambianie ukweli.

1. Ipe anwani mwafaka taarifa **(alama 1)**

2. Sigara husheheni idadi ya sumu? taja tatu kati ya hizo. **(alama 3)**

3. Eleza madhara mawili y uvutaji wa sigara **(alama 4)**

4. Eleza hila zinazotumiwa na makapuni ya sigara kuwavutia wateja. **(alama 4)**

5. Taja sababu tatu zinazowafanya vijana kuvuta sigara. **(alama 3)**

6. Eleza maana ya msamiati ufuatao kama uliyotumiwa katika makala.

i) Shinilizo - rika **ii)** Hunadi

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

SEHEMU B MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 50)

1. Sarufi ni nini. **(alama 2)**

2. Matamshi ya konsonanti za Kiswahili hubainishwa kutegemea vigezo vitatu. Vitage **(ala 4)**

3. a. Eleza maana ya.

i. sauti ghuna . **(alama 2)**

ii. Sauti hafifu. **(alama 2)**

b) Orodhesha konsonanti mbilimbili ambazo ni;

i. Vizuio – kwamiza

ii. Vipasuo vya kaakaa laini

iii. Vipasuo vya ufizo

4. a. Eleza maana ya silabi **(alama 2)**

b) Andika maneno mawilimawili yenye muundo wa silabi ya:

i) Irabu

ii) Silabi mwambatano

5. a. Bainisha aina za maneno katika sentensi zifuatazo. **(alama 2)**

i) Maria hufikiri sana siku hizi

b. Nomino hizi katika ngelo gani? **(alama 2)**

ii) Ukuti

7. Tulipokuwa tunaagana na sahibu Wangu aliniandikia anwani yake ambayo ni

slp 5 namsore **(alama 2)**

7. Andika kwa wingi.

Upepo wa kusini ulipeperusha bati la paa la nyumba na kuharibu kifaa muhimu. **(alama 2)**

8. Tunga sentensi yenye mapangilio ufuatao. **(alama 2)**

nomino+kivumishi+kitenzi+kielezi+kielezi

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

9. Tofautisha kati ya shadda na kiimbo

10. Taja na ueleze aina mbili za ala za matamshi toa mifano kwa kila aina.

11. Huku ukitoa mifano mwafaka, eleza maana ya"

i. Vitawe **ii.** Visawa:

12. Onyesha silabi inayowekewa shadda kwenye maneno yafuatayo.

i. Karatasi **iii**. Barabara (njia kuu)

ii. Barabara (shwari) **iv.** Barabara (njia kuu)

13. Eleza maana ya nasahau hizi

i. Jipalia makaa **ii.** Enda dalji

14. a. Tofautisha kati ya konsonanti na Irabu. **(alama1)**

b. Utamkaji wa irabu hu tegemea sifa tatu zitaje. **(alama3)**

SEHEMU C:

ISIMU – JAMII (ALAMA 15)

i. Eleza maana ya isimu jamii **(alama3)**

ii. Lugha ni nini. **(alama3)**

iii. Fafanua majukumu matano yanyotekezwa na lugha katika jamii. **(alama 10)**

SEHEMU D: FASIHI (ALAMA 20)

I. Eleza maana ya Fasihi simulizi. **(alama2)**

ii. Eleza dhima ya Fasihi katika jamii. **(alama5)**

iii. Andika tanzu zozote tatu za Fasihi simulizi. **(alama 3)**

iv. Eleza tofauti tano kati ya Fasihi simulizi. Andishi. **(alama10)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS KEYNOTE

KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 10

1. UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Nairobi, jiji kuu la Kenya ,ni jiji la maajabu na mastaajabu chungu nzima.Nadhari ya mtu anayewahi kuingia katika jiji hili kwa mara ya kwanza huvutiwa na huo mshehenеko wa majumba ya fahari, marefu ajabu, kiasi cha minazi mitano-sita ,iliyounganishwa kuelekea juu. mbinguni.

Jumba linalowavutia watu wengi ni lile Ia makongamano ya kimataifa Iiitwalo kwa Kiingereza *Kenyatta International Conference Centre* Jumba hili,hadi miaka michache iliyopita, ndilo lililokuwa refu zaidi mjini. Jumba lenyewe- lina ghorofa ishirini na tisa hivi ,usipohesabu hilo pambo kama kofia kileleni mwake,linalojulikana kama mwavuli. Hata hivyo ,miaka michache iliyopita jengo hili lilipitwa urefu na Mnara wa Nyakati (Times Tower).Mnara huo hasa ni jumba linaloafiki lakabu yake ya kikwaruza mawingu. Jumba hili lina ghorofa zisizopungua thelathini na mbili.

Mbali na majumba haya mawili ,kuna majumba mengine zaidi ya ishirini katikati ya jiji ambayo,japo mengine ni mafupi kiasi ,yana maumbo ya kustaajabisha kweli kweli.Hebu zingatia mwenyewe jumba Iiitwalo "mdomo wa kengele" au "bell —bottom" ambalo ni vioo vitupu ,toka chini hadi juu.Fauka ya ,umbo lake ni Ia kipekee ulimwenguni kote. Jumba hili lina kama miguu, kisha kiuno mithili ya kinu hivi japo si mviringo.Linapaa juu, mbali sana, likichukua umbo pana kuliko lilivyo chini;umbo la kifua pana kama kengele. Halafu rudia barabara; hizi hazina hesabu katikati ya jiji na ni pana, tena safi sana.Magari yanayotumia barabara hizi ni kochokocho,ya kila aina na yanashindania nafasi.

Ajabu kubwa ya Nairobi hata hivyo ni idadi ya watu. Hakuna hasa anayejua idadi kamili ya watu wa Nairobi ,lakini sio kupiga chuku ninaposema kwamba ,hasa nyakati za kuelekea kazini asubuhi ,kwenda kula chakula cha mchana ,kuelekea nyumbani baada ya kazi na kuvuka barabara wakati wa msongamano, watu hukanyagana .Mtu anayesema kwamba watu wa Nairobi ni wengi kama chungu ,au kama mchanga wa ufuo wa bahari, hatii chumvi.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Watu wa Nairobi, kwa tabia na mavazi, si kama watu wa kwingineko nchini Kenya .Watu hawa huvalia nadhifu sana.Wanawake ni warembo ajabu na hutengeneza nywele zao mithiIi ya hurulaini peponi.Wengi huvaa suruali ndefu. Kucha zao na midomo yao hupaka rangi maridadi sana. Huzungumza Kiswahili na Kiingereza takriban wakati wote.Wanawake wengi ajabu huendesha magari yao wenyewe ,jambo ambalo litakushangaza mara tu uingiapo jijini ,hasa kama ulilele wa ukidhani maskani mwafaka ya wanawake ni jikoni peke yake;yaani kuzingatia ile falsafa kuwa "kuoa ni kupata jiko".Wanaume nao huvaa suti safi ,maridadi na shingoni wamefunga tai stahiki yao.Wanaume hao huendesha magari na kuyaegesha karibu na afisi zao.Huingia afisini mwao kwa maringo na madaha, huku funguo za magari yao zikining'inia vidoleni. Hawa nao husema na Kiingereza kupitia puani, utadhani ni waingereza hasa.

Kwa upande mwingine ,watoto ni nadhifu kweli kweli hasa watoto wa shule.Hawa huvalia sare zilizofuliwa na kunyooshwa vizuri kwa pasi. Wake kwa waume ,shingoni huvalia tai. Watoto wa shule za Nairobi huongea Kiswahili, Kiingereza na *sheng*, ambayo ni msimu wao walioubuni.Msimu huu ni mchanganyiko wa Kiswahili,Kingereza na msamiati mchache wa lugha nyingine za Wakenya zisemwazo jijini Nairobi na vitongojini mwake.

Kwa jumla ,watu wote wa Nairobi hutembea kasi sana.Hawana hata wakati wa kutembea polepole na kuangazaangaza huku na huko.lwapo wewe ni mgeni jijini,ukizubaa utapigwa kumbo na waendelee na hamsini zao kama vile hapakutokea jambo.Hili linapojiri, usidhani limefanywa maksudi.La, hasha.Ni vile tu kwamba Wanairobi hawana muda wa kupoteza.

Maswali

(a) Toa kichwa mwafaka kwa makala haya **(ala 1)**

(b) **(i)** Tambua maajabu matatu yanayopatikana katika jiji la Nairobi. **(ala 3)**

(ii) Watu wa Nairobi wanajipenda kweli kweli, Fafanua **(ala 3)**

(c) **(i)** Kwa maoni yako, kwa nini majumba ya jiji la Nairobi yana majina au lakabu za Kiingereza? **(ala 1)**

(ii) Unafikiri ni kwa nini hasa wanawake wa Nairobi wanaonekana nadhifu? **(ala 2)**

(d) Watu wa Nairobi hukanyagana wakati upi ? **(ala 2)**

(e) Eleza maana ya maneno na tamathali za usemi zifuatazo. **(ala 3)**

(i) Nadhari **(ii)** Linaloafiki (iii) Waendelee na hamsini zao

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a. Andika vitamkwa vyenye sifa zifuatazo: **(alama 2)**

i) Kikwamizo cha meno

ii) kiyeyusho cha midomo

b. Taja vigezo vitatu vya kuainisha irabu **(alama 3)**

c. Onyesha vipashio vya lugha kuanzia kidogo hadi kikubwa **(alama 2)**

d. i). Shadda ni nini? **(alama1)**

ii) Tia shadda katika maneno yafuatayo: **(alama 2)**

Mbono (mti)

Barabara (sawasawa)

e. Taja ngeli za nomino zifuatazo **(alama 2)**

i) Ujinga

ii) Mashine

iii) Sukari

iv) Mti

f. Tunga sentensi ukitumia neno **kisabuni** kama: **(alama 2)**

i) Nomino

ii) kielezi

g. Bainisha virai katika sentensi ifuatayo **(alama 3)**

Mkulima stadi alilima vizuri kando ya mto.

h. **a.** Kiambishi ni nini? **(alama 1)**

b. Bainisha viambishi katika **Niliyemchorea** **(alama 3)**

i. Andika ukubwa wa maneno yafuatayo: (alama 2)

i) Mbuzi

ii) Kisu

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

j. Tunga sentensi moja moja kuonyesha matumizi ya alama za kuafikisha ulizopewa.

(alama 3)

a) Kistari kifupi

Ritifaa

b) Herufi kubwa

k. Andika upya sentensi zifuatazo katika hali ya kutendewa. **(alama 2)**

i) Tuju alivua samaki wengi.

ii) Mwalimu amempa mwanafunzi kitabu.

l. Changanua kwa mistari

Askari jela atamsindikiza mshukiwa mahakamani **(alama 4)**

m. Sahihisha sentensi zifuatazo.

Ile ni sungura ya nani? **(alama 1)**

Mwanafunzi ambaye aliyechelewa ameadhibiwa. **(alama 2)**

n. Yakinisha sentensi ifuatayo kwa udogo. **(alama 2)**

i) Nyumba yenyewe haikujengwa karibu na mto.

o. Andika kwa umoja. **(alama 1)**

Nyaraka zilizoandikwa zimepokelewa

p. Andika kinyume cha sentensi hii. **(alama 2)**

Mama aliketi baba alipoondoka.

3. ISIMU JAMII

a) Eleza sifa tano za lugha. **(alama 5)**

b) Lugha ina umuhimu gani katika jamii yako? **(alama 5)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

5. FASIHI SIMULIZI

a) Fafanua maana ya sanaa. **(Alama 2)**

b) Taja mifano mingine mitatu ya sanaa mbali na fasihi. **(Alama 3)**

c) Eleza tofauti sita kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. **(alama 6)**

d) Fafanua vipera vifuatavyo vya fasihi simulizi **(alama 4)**

i. Hekaya

ii. Visasili

iii. Hurafa

iv. Mighani

KILA LA HERI

Prefer Calling Amobi Group of Examiners@ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

CALL AMOBI GROUP OF EXAMINERS @ 0743 333 000 OR 0706 851 439 TO ACQUIRE :









